**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 4 No. 1 (2026): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v4i1.1549


# Umuhimu wa Ngano katika Jamii ya Wasukuma: Uchanganuzi wa Kijamii na Kitamaduni

**Janeth M. Balele[1] & Sydney E. Msonde[2]**
[1]*Education Department of the Dodoma Municipal Council, Tanzania*
[2]*Muhimbili University of Health and Allied Sciences, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-07-10
Kurekebishwa: 2025-11-20
Kukubaliwa: 2025-12-31
Kuchapishwa: 2026-02-05

**Maneno Muhimu**
Kisukuma
Ngano
Urithi
Utamaduni

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Balele, J. M. & Msonde, S. E. (2026). Umuhimu wa Ngano katika Jamii ya Wasukuma: Uchanganuzi wa Kijamii na Kitamaduni. *Journal of Kiswahili and Other African Languages,* 4(1), 1-12.

Copyright © 2026
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Makala hii ni sehemu ya utafiti uliofanyika kabla katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Ililenga kubainisha umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma wa Kahama, Mkoa wa Shinyanga, kwa muktadha wa kijamii na kitamaduni. Utafiti ulifanyika katika vijiji vya Mpera, Iyenze, Isagehe na mtaa wa Nyakato, ukihusisha wazee 64 wenye umri wa zaidi ya miaka 70 waliopatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa. Data zilikusanywa kupitia dodoso na mahojiano, ambapo zilichambuliwa kwa kutumia programu za SPSS kwa data za kitakwimu au za kiidadi, na ATLAS.ti kwa data za kimaelezo. Matokeo yalionesha kuwa washiriki wengi walikuwa na uelewa mkubwa kuhusu maana, umuhimu na matumizi ya ngano kama chombo cha kuimarisha maadili, mshikamano na kuhifadhi historia ya jamii. Wengine walitambua ngano kama visasili na visakale vinavyoeleza chimbuko la jamii, asili ya watu wake, na misingi ya mila na desturi zao. Aidha, utafiti huu umebainisha kwamba ngano ni urithi hai wa kitamaduni unaoendeleza utambulisho, maadili, na mshikamano wa jamii ya Wasukuma, sambamba na kutoa burudani na elimu kwa vizazi vinavyofuata. Utafiti unahitimisha kuwa ili kuhakikisha uendelevu wa urithi huu, ni muhimu kuweka mikakati ya kijamii na kielimu itakayohamasisha usimulizi wa ngano kwa vizazi vipya kupitia shule, makumbusho, na matamasha ya kitamaduni. Hatua hii itasaidia kuhifadhi na kuendeleza ngano za Kisukuma, na hivyo kuimarisha utambulisho na urithi wa kitamaduni wa Kiafrika.

## Utangulizi

Ngano ni mojawapo ya vipera muhimu zaidi katika fasihi simulizi vinavyobeba utambulisho na urithi wa jamii nyingi barani Afrika, ikiwemo jamii ya Wasukuma. Kwa mujibu wa Matteru (1983), ngano ni kipera maarufu katika fasihi simulizi ambacho ndicho kinachobeba utanzu wa hadithi. Fasihi simulizi ina vipera mbalimbali, lakini ngano ndicho kipera mama kinachotumika kuendeleza maadili, maarifa, na tajiriba za kijamii kupitia simulizi zinazopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hoja hii inafafanua nafasi ya ngano kama chombo cha mawasiliano na urithishaji wa utamaduni wa Kiafrika, hususan katika jamii zenye urithi wa simulizi kama Wasukuma. Maelezo ya Matteru (1983) yanaendeleza misingi iliyowekwa na Finnegan (1970) katika kazi yake mashuhuri ya *Oral Literature in Africa*, ambamo anasisitiza kwamba ngano ni kipera kikuu cha fasihi simulizi ya Kiafrika. Finnegan anaonesha kwamba utendaji (performance) ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi, na ndani ya ngano mara nyingi hujitokeza mwingiliano wa tanzu mbalimbali kama nyimbo, semi, maigizo, matambiko, na vichekesho. Mwingiliano huo una lengo la kuhakikisha ujumbe unawafikia walengwa kwa ufanisi na kwa namna inayochochea fikra, hisia, na maadili. Hivyo, ngano si hadithi

za kuburudisha pekee, bali ni nyenzo ya kijamii inayotumika kujenga mshikamano, maarifa, na falsafa za maisha ya jamii.

Uelewa wa dhima ya ngano unapanuliwa zaidi na Sengo (1987), ambaye anafafanua kwamba fasihi simulizi, ikiwemo ngano, hutekeleza dhima za kufunza, kuadilisha, kuelimisha, kukosoa, na kuburudisha. Dhima hizi zimekuwa kiini cha fasihi simulizi tangu jadi, zikichangia katika kuunda maadili na mitazamo ya kijamii. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, baadhi ya dhima hizi zimepanuka na kuakisi mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, na kitamaduni yanayoendelea kujitokeza. Hali hii inaashiria kuwa fasihi simulizi, na hasa ngano, ni hai na inabadilika kulingana na mahitaji ya jamii husika. Njogu na Chimerah (1999) wanasisitiza zaidi nafasi ya ngano kama kipera mama katika utanzu wa hadithi, na wanabainisha kuwa sifa yake kuu ni matumizi ya wahusika wanyama katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Aidha, kwa mtazamo wa waandishi wa Makala hii, Sungura na Fisi hujitokeza kama vielelezo vya maadili na tabia za kibinadamu zinazowasilishwa kwa njia ya sitiari na ucheshi; sungura huwakilisha ujanja na werevu, huku fisi akiashiria upumbavu na tamaa. Hata hivyo, mabadiliko ya kijamii na teknolojia yamechangia kuibuka kwa wahusika wenye sifa mseto—ujanja, wema, werevu, na udhaifu—jambo linaloonesha mageuzi ya kijamii na kiutamaduni katika simulizi za kisasa. Hivyo, ngano zinaendelea kubadilika sambamba na mabadiliko ya maisha ya jamii.

Kwa upande mwingine, Wamitila (2003) anabainisha kwamba ngano ndio msingi wa utanzu wa hadithi na husaidia kukuza fikra za watoto kupitia matumizi ya wahusika wa wanyama na mandhari ya porini. Uhalisia huu wa kimaigizo huwasaidia watoto kuendeleza fikra za ubunifu, kuelewa masuala ya kijamii, na kukuza uwezo wa kufikiri kwa kina. Hivyo, ngano zinachangia kukuza uelewa wa kijamii na kuendeleza vipaji vya kiakili na kiutamaduni miongoni mwa watoto na vijana.

Kwa jumla, mapitio haya ya maandiko yanaonesha kwamba ngano ni zaidi ya chombo cha burudani; ni hazina ya maarifa na nyenzo ya kijamii na kitamaduni inayotumika kuimarisha maadili, elimu ya jadi, na mshikamano wa jamii. Hata hivyo, tafiti nyingi zilizotangulia zimeelekeza mjadala katika dhima za jumla za fasihi simulizi bila kuchunguza kwa kina muktadha maalum wa jamii fulani, hususani jamii ya Wasukuma. Aidha, bado hakuna utafiti wa kina uliochunguza nafasi na umuhimu wa ngano katika kuendeleza maadili, elimu ya jadi, na urithi wa kitamaduni wa Wasukuma katika mazingira ya sasa yanayoathiriwa na mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia. Hivyo, makala hii inalenga kujaza pengo hilo kwa kuchambua kwa kina umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma kwa muktadha wa kijamii na kitamaduni, ili kubaini jinsi simulizi hizi zinavyoendelea kudumisha urithi wa jamii katika enzi za mabadiliko ya kisasa.

Utafiti huu kuhusu ngano za Wasukuma unahakikisha umuhimu wa ngano katika kuimarisha maadili, mshikamano, na uelewa wa kijamii, kama ilivyokuwa zamani. Kukumbatia mabadiliko ya kitamaduni na kijamii kunaleta mahitaji ya kuchunguza tena nafasi ya ngano, ili kubaini kama bado zinatoa mchango wa kijamii na kitamaduni kama zamani. Makala inachambua kwa kina umuhimu wa ngano kwa muktadha wa kijamii na kitamaduni, na jinsi zinavyochangia kujenga utambulisho wa jamii hiyo. Utafiti huu unauliza maswali makuu mawili:

1. Ni kwa namna gani ngano zinachangia kuimarisha maadili na mshikamano wa kijamii katika jamii ya Wasukuma?
2. Ni vipengele vipi vya kitamaduni vinavyojidhihirisha kupitia ngano za Wasukuma?

Utafiti huu unatoa mchango wa kielimu na kitamaduni kuhusu nafasi ya ngano kama urithi wa fasihi simulizi, ukionesha jinsi zinavyosaidia kuunganisha vizazi, kuhifadhi historia, na kuendeleza

utamaduni wa Wasukuma. Matokeo yanatoa mwanga kwa watafiti na watendaji kuhusu umuhimu wa kulinda na kuenzi urithi huu wa kifasihi kama sehemu ya utambulisho wa jamii ya Wasukuma.

**Utafiti Tangulizi**

Sehemu hii imewasilisha umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma kwa muktadha wa kijamii na kitamaduni, katika muktadha wa nafasi ya ngano katika jamii ya Wasukuma, dhima zake za kijamii na kitamaduni, na uhai wake katika muktadha wa kisasa.

**Nafasi ya Ngano katika Jamii ya Wasukuma**

Ngano zimekuwa uti wa mgongo wa utamaduni wa Wasukuma kwa karne nyingi, zikihusishwa moja kwa moja na maisha ya kila siku ya jamii hii. Kwa mujibu wa Masanja (2016), ngano si hadithi za kuburudisha pekee bali ni nyenzo muhimu za kijamii zinazotumika kufundisha maadili, kuendeleza urithi wa tamaduni, na kuunganisha vizazi kupitia usimulizi wa mdomo. Wazee hutumia ngano kama njia ya kutoa mafunzo ya kimaadili kwa watoto na vijana ili kuwajengea tabia njema, heshima, na utii kwa jamii. Aidha, ngano hutoa nafasi kwa jamii kuelewa historia na falsafa zao, hivyo kuimarisha utambulisho wa kijamii na hisia ya pamoja ya kuwa sehemu ya urithi wa kitamaduni (Gregory, 2024).

Kwa upande mwingine, nafasi ya ngano katika jamii ya Wasukuma ni pana zaidi ya mafunzo ya kijamii. Saanane na Faru (2017) wanabainisha kuwa ngano ni chombo cha mawasiliano kinachowezesha jamii kujadili masuala nyeti kama migogoro, umaskini, au mabadiliko ya kijamii kwa njia ya kifasihi. Kupitia masimulizi haya, jamii hujifunza namna ya kushughulika na changamoto mbalimbali bila kuvunja mshikamano wao. Utafiti wa Mnenuka (2020) unaonesha kuwa ngano, pia, ni hazina ya maarifa ya kiasili (indigenous knowledge), kwani hubeba taarifa kuhusu mazingira, wanyama, mimea, na falsafa za maisha ambazo ni muhimu kwa uendelevu wa jamii.

Kwa jumla, nafasi ya ngano katika jamii ya Wasukuma ni ya kijamii, kielimu, na kiutambulisho. Zinaimarisha uhusiano kati ya vizazi, zinahifadhi kumbukumbu za kihistoria, na zinahamasisha maadili ya pamoja. Bila ngano, jamii ya Wasukuma ingepoteza sehemu kubwa ya utamaduni wake wa mdomo na urithi wa kijamii unaoendeleza umoja na mshikamano wa kijamii.

**Dhima za Ngano za Kisukuma Kijamii na Kitamaduni**

Ngano za Kisukuma zimebeba dhima nyingi ambazo zinaakisi maisha, falsafa, na utamaduni wa watu wa kabila hili. Kijamii, ngano ni chombo cha malezi, zikitumika kama darasa la maadili linalowafundisha watoto umuhimu wa heshima, uadilifu, na ushirikiano katika jamii (Masanja, 2016). Kupitia wahusika wa hadithi, jamii hujifunza matokeo ya matendo mema na mabaya, jambo linalosaidia kudhibiti mwenendo wa kijamii. Kwa mfano, hadithi za wanyama kama sungura, fisi, au simba hutumiwa kuonesha mafunzo kuhusu ujanja, uvumilivu, au ubinafsi — dhamira ambazo zinaunda msingi wa elimu ya kijamii (Saanane & Faru, 2017).

Kitamaduni, ngano ni hifadhi ya kumbukumbu za kihistoria na zinasimulia uhusiano wa watu na mazingira yao. Zinaakisi falsafa za Wasukuma kuhusu uhusiano wa binadamu na dunia, na hutoa mafunzo juu ya thamani ya kazi, amani, na utu (Gregory, 2024). Ngano huchangia katika utunzaji wa lugha ya Kisukuma na kuimarisha umilisi wa vipengele vyake vya kiisimu, hususani matumizi ya misemo, nahau, na semi za kitamaduni zinazojenga utambulisho wa lugha na jamii husika (Gregory, et al., 2024; Gabriel, 2023). Zaidi ya hayo, ngano ni jukwaa la kijamii linalounganisha jamii kupitia shughuli kama masimulizi ya pamoja, matamasha ya kitamaduni, na michezo ya kuigiza inayohusisha maudhui ya ngano (Paschal, 2016). Hivyo, dhima za ngano za Kisukuma ni pana—zinafundisha, zinaburudisha, zinahifadhi, na kuendeleza utamaduni. Kwa mtazamo wa kijamii na

kitamaduni, ngano hufanya kazi kama mwongozo wa maadili na dira ya urithi wa Wasukuma unaoendelea kuishi katika simulizi za mdomo.

**Uhai wa Ngano katika Muktadha wa Kisasa**

Licha ya umuhimu wake mkubwa, uhai wa ngano za Kisukuma unakabiliwa na changamoto nyingi katika enzi ya kisasa. Maendeleo ya teknolojia, upanuzi wa miji, na ushawishi wa tamaduni za nje vimesababisha kupungua kwa usimulizi wa ngano katika familia na jamii (Gregory, 2024). Vijana wengi wa Kisukuma wamezama katika matumizi ya mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, hivyo kupoteza hamasa ya kushiriki katika simulizi za jadi (Mnenuka, 2020). Aidha, mfumo wa elimu wa kisasa haujatoa nafasi ya kutosha kwa fasihi ya mdomo kama nyenzo ya kujifunzia maadili na utamaduni wa ndani, hali inayochangia kufifisha uhai wa ngano.

Hata hivyo, kuna matumaini makubwa ya kuzifufua ngano katika muktadha wa kisasa. Teknolojia kama video, podcast, na tovuti za kielimu inaweza kuwa daraja la kuhifadhi na kusambaza ngano, kwa mujibu wa Saanane na Faru (2017). Vyuo vikuu na mashirika ya kitamaduni pia yanaweza kuanzisha programu za utafiti na maonesho ya ngano ili kuendeleza urithi huu (Paschal, 2016). Uhai wa ngano sasa unategemea ubunifu wa kijamii na kielimu kuziunganisha na muktadha wa kisasa bila kupoteza asili yake. Wasukuma wanapaswa kutumia mbinu za kidijitali na kielimu kuhakikisha ngano zinaendelea kuwa nyenzo ya maadili, urithi, na utambulisho wa kijamii kwa vizazi vijavyo.

**Methodolojia ya Utafiti**

Utafiti ulifanyika Kahama, Shinyanga, kwa kuchagua kwa nasibu kata nne kati ya 20, na vijiji vya Mpera, Iyenze, Isagehe, na mtaa wa Nyakato, na wazee wa zaidi ya miaka 70 kwa usampulishaji lengwa. Umri wa wazee ulikaguliwa kwa mahojiano ya familia na kumbukumbu rasmi zilitokana na Sensa ya mwaka 2022. Mbinu hizi ziliwezesha ukusanyaji wa data bora, na hali ya uwepo wa malikale kama nyayo za Ng'wanamalundi na Bao ilifanya eneo hili kuwa maalum kwa utafiti huu. Katika utafiti huu, msingi wa sampuli ulijumuisha wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 70 waliokuwa wanaishi katika vijiji tajwa hapo juu. Wazee hawa ni hazina ya maarifa ya asili, na wanaufahamu wa kina kuhusu maudhui, maana, na umuhimu wa ngano katika jamii yao.

Wakati wa kufanya utafiti huu, kulikuwa na wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 70 wapatao 68 katika eneo la utafiti. Idadi hii, ilipatikana kutoka rekodi za ofisi za kata nne zilizochaguliwa. Rekodi hizo zilitokana na Sensa iliyofanyika mwaka 2022. Kwa kutumia taarifa hizi rasmi, tulihakikisha kuwa wote walitambuliwa kwa usahihi na kuingizwa kwenye utafiti. Aidha, watafiti walitumia fomula ya Yamane (1967) ili kupata ukubwa wa sampuli hitajika.

$$n = \frac{N}{1 + Ne^2}$$

Ambapo:
n ni saizi ya sampuli,
N ni ukubwa wa idadi ya watu, na
e ni kiwango cha usahihi.

Kulingana na fomula hapo juu, sampuli ya wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 70 kutoka vijiji vinne ilikuwa 58, iliongezwa kwa asilimia 10 kwa ajili ya usalama wa majibu. Jumla ya washiriki 64 walihusishwa katika ujazaji wa madodoso kwa usampulishaji lengwa. Aidha, utaratibu wa uteuzi kulingana na kigezo (criterion-based sampling) kama ulivyoelezwa na Forero et al. (2018) ulitumika kuwachagua wazee nane (8) kwa ajili ya mahojiano ya kina, ambapo uteuzi huo ulizingatia sifa mahsusi zikiwemo uzoefu wao kuhusu mada ya utafiti, uwezo wa kutoa taarifa kwa uwazi, na utayari wao wa kushiriki katika mahojiano. Utafiti huu ulikuwa na wazee waliokuwa na uzoefu wa kutumia ngano za jamii ya Kisukuma kutoka vijiji vya Mpera, Iyenze, Isagehe na mtaa wa Nyakato.

Watafiti walitumia dodoso na mahojiano kukusanya data. Walitengeneza dodoso lililopitiwa na wataalamu na kufanya majaribio kwa washiriki nane wasio sehemu ya utafiti. Toleo la mwisho la dodoso lilitumika kukusanya maoni kutoka kwa washiriki 64 (wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 70) kuhusu umuhimu wa ngano kwa jamii ya Wasukuma na jinsi zinavyochangia utambulisho wa jamii hiyo. Madodoso 28 yalijazwa kikamilifu, kuwezesha uchambuzi wa takwimu. Kwa wazee 10 ambao hawakuweza kusoma na kuandika, madodoso yao yalijazwa moja kwa moja na watafiti mbele ya wawakilishi wa familia zao, na majibu yao yaliandikwa kwa usahihi kwenye madodoso husika. Baada ya ujazaji huo wa madodoso, wazee walisomewa maelezo yao ili kujiridhisha kama maelezo waliyotoa yalinukuliwa kwa usahihi. Hii ilihakikisha kuwa data zote zilikuwa kamili na zinaweza kutumika katika uchambuzi wa takwimu.

Kwa upande mwingine, washiriki nane (8, wawili kutoka kila kijiji) walialikwa kushiriki katika mahojiano. Aidha, washiriki hao walichaguliwa kwa makusudi miongoni mwa washiriki 64 kwa kuzingatia utayari wao wa kushiriki katika mahojiano; ambapo ukusanyaji wa taarifa ulifikia kiwango cha ukamilifu wa maelezo (*data saturation*) baada ya kufanya mahojiano na washiriki wanne. Mahojiano hayo yalilenga kutathmini mitazamo ya washiriki kuhusu umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma, hususan katika muktadha wa kijamii na kitamaduni. Kila mahojiano yalidumu kwa wastani wa dakika 10. Rekodi za sauti zilinaswa na kisha kutafsiriwa kwa maneno halisi, huku washiriki waliokuwa wanajuwa kusoma na kuandika walialikwa kupitia maandiko ya mahojiano yao. Aidha, washiriki waliokuwa hawajui kusoma walisomewa nukuu ya mahojiano yao ili kuhakikisha kuwa maoni yao yamenukuliwa kwa usahihi.

Uchambuzi wa data ulifanywa kwa kutumia SPSS 23 kuonyesha asilimia na mkengeuko wa kawaida, kuonyesha maoni kuhusu umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma kwa muktadha wa kijamii na kitamaduni na jinsi zinavyosaidia kuunda utambulisho wa jamii. Watafiti pia walitumia uchambuzi wa maudhui kwa data kutoka mahojiano na programu ya ATLAS.ti kwa ajili ya usimbaji. Misimbo ilijumuisha maoni ya wazee na kuunganisha misimbo sawa kuwa mada kuu na ndogo. Usimbaji pia ulihisiwa na msimbaji huru kwa ukaguzi na vihatarishi vya makubaliano vilifanyika ili kudhibiti tofauti. Vitatizo vya usimbaji vilitatuliwa na watafiti wakiendeleza na kupanga upya data na misimbo kwa kutumia programu ya usimbaji ili kupata uelewa wa kina kuhusu maoni kuhusu umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma.

**Matokeo ya Utafiti na Mjadala Wake**
Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti wa ngano katika jamii ya Wasukuma, ukiangazia muktadha wa kijamii na kitamaduni. Mjadala unaofuata unalenga kutafsiri matokeo kwa mtazamo wa fasihi simulizi na namna ngano zinavyosaidia kuleta utambulisho wa jamii hiyo.

**Tafasiri ya Ngano katika Jamii ya Wasukuma**
Watafiti walikusudia kutathimini kiwango cha ufahamu wa washiriki kuhusu namna ngano zinavyochangia kuimarisha maadili ya jamii ya Wasukuma. Hivyo, Washiriki waliulizwa kueleza namna gani ngano zinachangia kuimarisha maadili na mshikamano wa kijamii katika jamii ya Wasukuma. Matokeo ya swali hili yalionesha kuwa washiriki wengi walieleza kuwa wanafahamu tafsiri na matumizi ya ngano katika jamii yao. Ili kupata uelewa wa kina zaidi, watafiti waliwauliza washiriki kujibu maswali ya chaguo nyingi kwa kutumia kipimo cha Likert (1 = Sina ufahamu kabisa, 5 = Nina ufahamu mkubwa). Majibu ya washiriki kwenye Jedwali Na. 1 yanathibitisha kuwa 71% walikuwa na ufahamu wa juu kuhusu maana ya ngano kwa Wasukuma, 71% walikuwa na ufahamu wa wastani, na 2.6% walikuwa na ufahamu wa chini. Hakuna aliyejipima kiwango cha chini kabisa. Hii inaonyesha kuwa wengi wanamwelewa vyema maana ya ngano katika jamii ya Wasukuma.

*Jedwali Na 1: Kiwango cha Ufahamu Juu ya Ngano*

| **Kauli** | **Pima kiwango chako cha ufahamu juu ya ngano** | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Ninajua maana ya ngano katika jamii ya Wasukuma | 0 | 1 | 2 | 8 | 27 |
| Ninajua umuhimu wa ngano katika kuwasilisha maadili na historia. | 1 | 0 | 0 | 7 | 30 |
| Ninajua mifano ya ngano inayotumika katika jamii ya Wasukuma. | 0 | 0 | 1 | 9 | 28 |
| Ninajua jinsi ngano zinavyosaidia katika mshikamano wa kijamii. | 1 | 1 | 0 | 11 | 25 |
| Ninajua athari ziletwazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia | 1 | 2 | 5 | 6 | 24 |

Aidha, kwa kauli ya pili, "Ninajua umuhimu wa ngano katika kuwasilisha maadili na historia," matokeo yanaonyesha kuwa 30 (79%) walionesha uelewa wa hali ya juu, 7 (18.4%) walionesha kuwa na uelewa wa hali ya juu, na mmoja (2.6%) alikuwa na uelewa wa chini. Hii ni ishara kuwa umuhimu wa ngano katika kuwasilisha maadili na historia unafahamika sana jamii ya Wasukuma. Pia, kwa kauli ya "Ninajua mifano ya ngano inayotumika katika jamii ya Wasukuma," matokeo yanaonyesha kuwa 28 (73.7%) walionesha uelewa wa hali ya juu, 9 (23.7%) walionesha kuwa na uelewa wa hali ya juu, na hakuna aliechagua viwango vya chini kabisa. Hii inaonyesha washiriki wana ufahamu mzuri kuhusu mifano ya ngano zinazotumika jamii ya Wasukuma.

Kauli ya nne inathibitisha kuwa washiriki wengi (65.8%) wana ufahamu mkubwa kuhusu mchango wa ngano katika mshikamano wa kijamii, huku wachache (28.9%) wakiwa na kiwango cha juu sana na wachache (5.3%) wakichagua viwango vya chini kabisa. Uchambuzi wa kauli ya tano unaonyesha utofauti wa ufahamu kuhusu athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia, ambapo asilimia 63.2% wana ufahamu mkubwa, asilimia 15.8% wanaendelea na kiwango cha juu, na asilimia 21% wana ufahamu mdogo, ikionyesha kuwa ufahamu kuhusu athari za sayansi na teknolojia ni mdogo ikilinganishwa na maoni mengine. Kwa ujumla, washiriki wanamefahamu vizuri vipengele vya msingi vya ngano za Kisukuma, ikiwa ni pamoja na maana, umuhimu, mifano, na mchango wake katika kuimarisha mshikamano wa kijamii, ingawa ufahamu kuhusu athari za sayansi na teknolojia unahitajika kuimarishwa.

Matokeo yanaonyesha wengi wana uelewa wa maana ya ngano kwa jamii ya Wasukuma, ikihifadhi utamaduni na maadili. Utafiti wa Mulokozi (2006) unaonyesha jamii za Kiafrika zinatumia fasihi simulizi kwa malezi, na wazee wa Kisukuma wanafahamu maana na matumizi ya ngano. Washiriki pia walihusiana na ngano na maadili na historia, kama alivyogundua Wamitila (2003), akisema ngano si tu hadithi za kuburudisha bali nyenzo za kujenga tabia, mshikamano wa kijamii, na urithi wa historia kutoka kizazi hadi kingine. Katika jamii ya Wasukuma, ngano zinawasilisha hekima za mababu na kuelekeza vijana, kama ilivyo kwa jamii nyingine za Kiafrika. Matokeo yanaonyesha washiriki wana ufahamu mzuri wa mifano ya ngano zinazotumika, zikionyesha kuwa bado zinatumika kwa kiasi kikubwa, hasa miongoni mwa wakazi wa eneo hilo. Utafiti wa Mnenuka (2020) unathibitisha kuwa jamii zinazohifadhi urithi kupitia masimulizi kama ngano, methali, na hadithi za jadi. Hivyo, ngano bado ni sehemu muhimu ya maisha ya Wasukuma.

Aidha, utafiti huu unaonyesha kwamba washiriki wengi wanatambua mchango wa ngano katika kuimarisha mshikamano wa kijamii, ikithibitisha kuwa ngano ni kiungo muhimu cha kuunganisha jamii, kama Simiyu (2019) alivyosema, kwamba fasihi simulizi husaidia kujenga mshikamano kwa kuhimiza ushirikiano wa kijamii, mshikamano, na maadili mema. Katika jamii ya Wasukuma, ngano husaidia kuunganisha vizazi tofauti kwa kuwapatia vijana fursa ya kujifunza kutoka kwa

wazee kupitia masimulizi ya kifasihi. Utafiti unaonyesha kuwa jamii ya Wasukuma ina uelewa mzuri wa maana na umuhimu wa ngano, huku ikitambua nafasi yake katika mshikamano wa kijamii. Watafiti waliwauliza washiriki kueleza mitazamo, uzoefu, na ufahamu wao kuhusu ngano, lengo likiwa ni kutoa fursa kwa washiriki kueleza mawazo yao kwa undani. Washiriki walikuwa na mitazamo mchanganyiko. Wakati wengi wa washiriki waliohojiwa 3(75%) waliona ngano kama hadithi fupifupi, baadhi 1(25%) walichukulia ngano kama visasili na wengine waliona ngano kama visakale, kama inavyooneshwa katika kifungu kilichopo hapa chini:

> Ngano ni mazungumzo au masimulizi yanayosimuliwa na bibi, babu au mtu mzima ambaye husimulia matukio mbalimbali yaliyofanyika au yanayofanywa na binadamu kupitia wanyama wakiwakilisha matendo mazuri au mabaya kwa jamii husika. Masimulizi hayo husimuliwa watoto, wajukuu, na watu wengine wakiwa wamekaa kando kando au pembeni mwa nyumba au wakiwa wanaota moto huku wakisimulia na kusikiliza masimuliz (shikome) usiku baada ya kazi (P02:15; 12:12)[1].

Inaonesha kwamba mshiriki huyo alikuwa anaeleza juu ya ngano kama hadithi fupi fupi. Kwa mfano, maelezo hayo hapo juu yanaonesha kwamba wapo washiriki wanaoamini kuwa ngano ni hadithi fupi fupi au masimulizi yanayotolewa na bibi, babu, au mtu mzima akisimulia watoto na wajukuu wakiwa wamekaa kando kando au pembeni mwa nyumba au wakiwa wamekaa karibu na moto (shikome) nyakati za jioni baada ya kazi. Masimulizi hayo hutolewa kwa lengo la kutoa mafunzo, kuonya, na kuburudisha wasikilizaji na jamii kwa ujumla. Wahusika wa masimulizi wakiwa ni watu wazima au wazee. Watafitiwa waliojibu kwa mtazamo huo, wao, walijikita katika namna ya uwasilishaji kwamba kuna mazungumzo kati ya mwasilishaji na mpokeaji (fanani na hadhira). Sambamba na mtazamo huu, wengine walijikita katika mtazamo wa ngano kama visasili:

> Ngano ni matambiko yanayofanyika katika miti mikubwa, mawe, makaburini ili kuomba kwa Mungu na kupitia wahenga wetu ili waweze kutoa baraka na kutubu makosa waliyokosea. Pia, wanapo fanya matambiko hueleza chimbuko la jamii yao na namna jamii ilivyofika katika eneo kwa kutaja koo zao za asili. Ngano husaidia kueleza asili ya jambo lisiloelezeka kama mauti, jando (tohara), unyago, ndoa na imani nyingine (P02:23; 14:14).

Nukuu inaonyesha washiriki wakielezea ngano kama visasili, wakitokana na historia ya jamii na tamaduni, kuelezea asili ya mambo kama mauti na imani. Wameunga mkono kwamba visasili ni muhimu kwa jamii ya Wasukuma kudumisha mila na desturi. Zaidi ya hayo, washiriki wachache sana 1(25%), walichukulia ngano kama visakale na baadhi yao walikuwa na mitazamo ifuatayo:

> Ngano husimulia matukio ya kale yaliyofanywa na babu zetu, ambayo yanaweza kuwa ya kweli au ya kubuni. Mara nyingi husimulia kuhusu wafalme, koo za utawala, kumbukumbu za koo fulani, magonjwa, vita, na njaa za zamani. Wahusika wake mara nyingi huwa ni binadamu ambao hupewa uwezo mkubwa au mdogo kulingana na matukio yaliyosimuliwa (P01:25; 14:14).

[1]Nambari zinazofuata kila nukuu (mfano: P02:15; 12:12) zinaonesha sehemu ya hati ambapo nukuu hiyo inaweza kufuatiliwa. Herufi na nambari mbili za kwanza zinaashiria nambari ya utambulisho (ID) ya nukuu na wakati ilipotengenezwa. Kwa mfano, P02:15 inamaanisha nukuu hiyo ilitokana na hati ya msingi namba 02 na ilikuwa nukuu ya Kumi na Tano iliyotengenezwa katika hati hiyo. Nambari mbili za mwisho katika kila nukuu zinaonesha namba ya aya ambapo sehemu iliyokodishwa ipo. Kwa mfano, katika nukuu ya kwanza, 12:12 inamaanisha nukuu inaanza katika aya ya 12 na kumalizika katika aya ya 12.

Baadhi ya washiriki walielewa ngano kama vitu vihusuvyo masuala ya visakale, zinahusiana na simulizi za kihistoria, za kweli au za kubuni, mara nyingi zikihusu historia ya wafalme, koo za utawala, magonjwa, vita, na njaa. Visakale huwa ni hadithi zinazolenga kuonya na kuburudisha jamii kuhusu tukio fulani, ili kuzuia au kukomesha linapotokea. Watafiti wanasema ngano ni matukio ya kihistoria, yaliyokwisha tokea au yanatarajiwa kutokea, na ingawa washiriki waliona ngano kama hadithi fupi, visasili, na visakale, ilihali ni muhimu kwa mtafiti kufanya tathmini ya ufahamu wao kuhusu makundi ya ngano katika jamii ya Wasukuma.

Utafiti huu unaonesha kwamba washiriki walikuwa na mitazamo tofauti kuhusu maana ya ngano. Baadhi waliitazama kama hadithi fupifupi, wengine kama visasili, na wengine kama visakale. Mtazamo huu unalingana na tafiti za zamani zinazothibitisha kuwa dhana ya ngano ni pana na hutegemea muktadha wa kijamii na kiutamaduni (Mbunda, 1992). Kwa mfano, tafiti za Senkoro (2011) na Simiyu (2011), zinaeleza kuwa ngano ni masimulizi yanayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo na hutegemea wahusika wa jamii husika. Hii inaendana na maelezo ya mshiriki 1, aliyesema kuwa ngano ni masimulizi yanayotolewa na wazee kwa watoto na wajukuu kwa madhumuni ya kutoa mafunzo na burudani. Tafiti za hivi karibuni zinaunga mkono mtazamo huu, zikionyesha kuwa ngano huchangia katika ujenzi wa maadili ya jamii na urithishaji wa maarifa ya kitamaduni (Khamis, et al, 2008).


Aidha, utafiti huu unathibitisha nadharia ya Oyoyo (2013) kuhusu urazini wa ngano, ambapo inatajwa kuwa ngano zina miundo inayojirudia na zinaweza kuhusisha vipengele vya kufundisha maadili au kueleza asili ya jamii. Washiriki waliotambua ngano kama visasili walieleza kuwa zinaeleza asili ya jamii, mila, na desturi, jambo ambalo linafanana na tafiti zilizopita zinazoonesha kuwa visasili vina mchango mkubwa katika kuhifadhi historia na utambulisho wa jamii (Mbarouk, 2015). Aidha, utafiti kama wa Songoyi (1997) unaonesha kuwa ngano, hasa katika jamii za Kiafrika, hutumika kama njia ya kuimarisha mshikamano wa kijamii na kuendeleza urithi wa kitamaduni.

Hata hivyo, matokeo haya yanatofautiana na baadhi ya tafiti zilizopita. Kwa mfano, Mbarouk (2015) alieleza kuwa ngano, mara nyingi, hutazamwa kama masimulizi ya kubuni, bila uhusiano na historia halisi ya jamii. Kinyume chake, washiriki wa utafiti huu waliona kuwa ngano zina uhusiano mkubwa na historia, hasa kwa wale waliotambua ngano kama visakale. Matokeo haya yanaendana na nadharia za kiantropolojia zinazodai kuwa jamii hutumia ngano kama njia ya kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria na matukio muhimu (Songoyi, 1997). Tafiti za hivi karibuni kama ule wa Mbarouk (2015), zinathibitisha kwamba ngano zinaweza kuwa chanzo cha kihistoria kinachosaidia kuelewa mabadiliko ya jamii na namna jamii zinavyokabiliana na changamoto zao.

**Umuhimu wa Ngano katika Jamii ya Wasukuma**

Kwa kuzingatia umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma, makala hii inajibu maswali makuu mawili yanayoangazia namna ngano zinavyochangia kuimarisha maadili na mshikamano wa kijamii, pamoja na vipengele vipi vya kitamaduni vinavyojidhihirisha kupitia ngano za jamii hii. Hivyo, watafiti waliwauliza wazee wa Kisukuma kupitia dodoso kueleza ufahamu wao kuhusu umuhimu wa ngano katika kabila la Wasukuma. Matokeo ya utafiti yanatoa tathmini ya wazee kuhusu mchango wa ngano katika urithi na usambazaji wa maarifa, historia, na maadili. 11 (29%) walisema ni sehemu muhimu ya urithi wa utamaduni wa Wasukuma, na 9 (24%) waliona muhimu kwa kuhamisha maarifa na historia, hivyo kusaidia kudumisha utambulisho wa jamii.

*Mchoro Na 1: Umuhimu wa ngano katika jamii ya Wasukuma*




Matokeo ya utafiti huu yanaonesha, pia, kwamba wazee 7(18%) waliziona ngano kama chombo muhimu kinachoweza kutoa elimu isiyo rasmi iletayo maadili na tabia njema kwa watu. Aidha, wazee 6 (16%) walionesha mtazamo wao kwamba ngano huchangia katika utoaji wa burudani, huku wengine 3 (8%) wakitambua umuhimu wa ngano kama chombo cha kufundisha lugha ya Kisukuma, hivyo kusaidia kuhifadhi na kukuza matumizi ya lugha hiyo.

Sambamba na hayo, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wazee 2 (5%) waliona ngano kama chombo cha kuimarisha mshikamano wa kijamii, hasa katika mikusanyiko ya kifamilia na kijamii. Hali hii inatokana na uwezo wa usimulizi wa ngano kuwaleta watu pamoja, na hivyo kuimarisha mahusiano na mshikamano wa kijamii. Kwa ujumla, ngano ni urithi muhimu wa jamii ya Wasukuma, unaochangia katika kudumisha utambulisho wa kiutamaduni, mshikamano wa kijamii, na maadili ya kijadi.

Hivyo, utafiti huu unaonesha kuwa ngano zina nafasi muhimu katika jamii ya Wasukuma, hasa katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni na maadili ya kijamii. Aidha, ngano si hadithi za kubuni tu, bali ni chombo cha kuhamisha maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Mbarouk, 2015; Mbunda, 1992). Matokeo haya yanalingana na uchambuzi wa Mbarouk (2015), ambaye anaonesha kuwa hadithi hueleimisha na kuelekeza jamii katika maadili mema. Mbali na jukumu la elimu isiyo rasmi, ngano pia zina mchango mkubwa katika burudani na utunzaji wa lugha ya Kisukuma. Utafiti huu unaonesha kuwa ngano zilitumika hasa wakati wa mapumziko baada ya shughuli za kilimo, jambo linalothibitishwa na Musembi na Mahero (2022) ambao wanabainisha kuwa fasihi simulizi ina nafasi muhimu katika maisha ya jamii zinazojihusisha na kilimo.

Aidha, ngano husaidia kuhifadhi na kukuza matumizi ya lugha ya Kisukuma (Jackson, 2014; Mlacha, 1995), na huleta mchango mkubwa katika mshikamano wa kijamii kwa huzileta familia pamoja wakati wa usimuliaji, hivyo kuimarisha mahusiano ndani ya jamii. Matokeo haya ya utafiti yanaendana na utafiti wa Mbarouk (2015), unaoeleza kuwa fasihi simulizi huchangia katika mshikamano na utambulisho wa jamii. Kwa hiyo, matokeo haya yanaonesha kuwa ngano si hadithi za kuburudisha tu, bali ni nyenzo muhimu ya kuhifadhi utamaduni na kufundisha maadili, kukuza lugha, na kuimarisha mshikamano wa kijamii, kama inavyothibitishwa na tafiti mbalimbali katika nyanja ya fasihi simulizi. Kadhalika, matokeo haya yalilingana na yale yaliyopatikana wakati wa mahojiano na wazee wa kimila katika jamii ya Kisukuma walipoulizwa kueleza umuhimu wa makundi ya ngano na jinsi zinavyotumika katika jamii yao. Kwa ujumla, wengi wa wazee

waliohojiwa 3(75%) waliripoti udumishaji wa mambo ya kitamaduni, urithishaji wa mila na desturi kwa vizazi vyao, pamoja na kuleta mshikamano na kukuza maadili katika jamii yao.

> Ngano ni muhimu kwa sababu hutupatia mafundisho ambayo husaidia katika maisha yetu na kutatua mambo mbalimbali yanayojitokeza, pia tulisimuliwa juu ya kuabudu katika miti, milima ili kumwomba Mungu ashushe mvua na kuondoa mikosi katika jamii. Kwa kufanya hivyo, koo nyingi ziliweza kuungana pamoja, kuwasilisha mila na desturi za jamii (P03:12; 36:37).

> Kupitia masimulizi ya ngano yanatufanya tuwe na umoja katika kushirkiana kama vile kulima, kuvuna mazao, harusi na misiba. Hivyo, ngano huchangia katika kukuza maelewano, kufahamiana, na kudumisha undugu ndani ya kabila la Wasukuma (P03:12; 50:50).

> Masimulizi ya ngano yanatufundisha namna mababu zetu walivyokuwa wanathamini mila na desturi za Kisukuma, ngano nyingi tulisimuliwa kwa Kisukuma. Mandhari waliyokuwa wakizungumzia zaidi katika ngano ni ya msituni, miti, mawe makubwa, na milima (P04:10; 21:21).

Kulingana na uchambuzi wa vifungu vya hojaji hapo juu, wazee wa Kisukuma wanaonyesha aina mbalimbali za ngano zinazotumiwa kwa malengo tofauti, na pia wanasisitiza umuhimu wa ngano kuhifadhi na kuendeleza tamaduni, kuhamisha maarifa kwa vizazi vijavyo, na kuleta uelewa na uadilifu katika jamii. Baadhi ya wazee walitilia mkazo uhusiano wa ngano na burudani na mchango wake katika kuimarisha mshikamano wa kijamii. Uchambuzi wa tafiti nyingine unaonyesha masimulizi ya ngano za Kisukuma yana mchango mkubwa katika kuendeleza umoja, kudumisha mila, na kuelezea historia na mitazamo ya zamani. Tafiti kama za Raphael (2015) na Wanjala (2015) zinaonyesha masimulizi hayo kuwa njia muhimu ya kuelimisha vijana kuhusu mila, desturi, na uhusiano wa kijamii.

Aidha, Mulokozi (2006) anasisitiza kuwa masimulizi ya ngano ni urithi wa tamaduni na yanatoa fursa ya kufundisha maadili kama ushirikiano, mshikamano, na kuthamini historia. Tafiti zilizoasisiwa zinaonyesha umuhimu wa ngano katika kujenga umoja kati ya koo, na kutoa nafasi ya kushiriki shughuli za kijamii kama kilimo, harusi, na misiba, hivyo kuendeleza undugu wa kabila.

Vilevile, tafiti za Khamis na wenzake (2008) zinaonyesha kwamba masimulizi ya ngano yanashirikisha maadili na mila, na kutoa ufahamu wa maisha ya mababu. Wamitila (2003) anasema kuwa kupitia masimulizi ya ngano, vijana wanapata mtazamo wa kisasa kuhusu maisha ya jadi na fursa ya kushiriki urithi wa tamaduni. Maudhui haya yanaonyesha kuwa masimulizi ya ngano yanahusiana na mazingira kama misitu, miti, na milima, sehemu ya utamaduni wa Kisukuma. Tafiti zinaonyesha kuwa masimulizi ya ngano ni chombo muhimu cha kuendeleza mila, desturi, na mshikamano wa kijamii, pia ni njia muhimu ya kuhamasisha umoja na kuelewa historia na utamaduni wa Wasukuma. Hivyo, ngano za Kisukuma ni urithi muhimu unaosaidia kudumisha tamaduni, mshikamano, maadili, na uhifadhi wa lugha kupitia elimu isiyo rasmi na burudani.

**Hitimisho**

Utafiti huu umeonesha kwa kina umuhimu wa ngano kama chombo cha kijamii na kitamaduni katika jamii ya Wasukuma. Kwa muktadha wa kijamii, ngano zimebainika kuwa nyenzo muhimu katika kujenga na kuimarisha mshikamano wa kijamii, kukuza maadili, na kuimarisha mawasiliano kati ya vizazi. Kupitia usimulizi wa ngano, vijana hupata uelewa wa kina kuhusu desturi, taratibu, na falsafa zinazounda msingi wa maisha ya jamii yao. Hivyo, ngano hufanya kazi kama daraja

linalounganisha vizazi, huku zikiwa chombo cha kujifunza na kufundishia maadili mema, nidhamu, na wajibu wa kijamii.

Kwa upande wa kitamaduni, ngano zimebainika kuwa kiini cha utambulisho wa jamii ya Wasukuma. Zinahifadhi kumbukumbu za kihistoria, zinabeba falsafa za mababu, na kuakisi mtazamo wa Wasukuma kuhusu maisha, utu, na maadili ya kijamii. Kupitia ngano, jamii huweza kuendeleza urithi wa tamaduni zake na kuuhamishia kwa vizazi vijavyo kwa njia ya ubunifu na usimulizi. Hata hivyo, utafiti huu umeonesha changamoto ya kupungua kwa kasi ya usimulizi wa ngano kutokana na mabadiliko ya kijamii, kiteknolojia, na kimfumo, hali inayohatarisha mwendelezo wa urithi huu muhimu.

Kwa kuzingatia matokeo haya, inashauriwa kuwepo kwa mikakati endelevu ya kijamii na kielimu itakayohamasisha urithishaji wa ngano kupitia programu za shule, semina, na matukio ya kitamaduni. Hatua hizi zitasaidia kulinda, kuendeleza, na kufufua urithi wa ngano kama nyenzo ya kukuza utambulisho wa kijamii na kitamaduni wa Wasukuma. Vilevile, tafiti zijazo zinapaswa kuchunguza mbinu shirikishi za kidijitali na kijamii ambazo zinaweza kutumika katika kuhifadhi na kusambaza ngano katika zama za sasa za mabadiliko ya kiteknolojia

**Marejeo**

Allahyari, T., Rangi, N. H., Khosravi, Y., & Zayeri, F. (2011). Development and Evaluation of a New Questionnaire for Rating of Cognitive Failures at Work. *International Journal of Occupational Hygiene*, 3(1), 6-11.

Campbell, S., Greenwood, M., Prior, S., Shearer, T., Walkem, K., Young, S., Bywaters, D., & Walker, K. (2020). Purposive Sampling: Complex or Simple? Research Case Examples. *Journal of Research in Nursing*, *25*(8), 652–661.

Elfil, M., & Negida, A. (2019). Sampling Methods in Clinical Research: An Educational Review. *Archives of Academic Emergency Medicine*, *7*(1), 3–5.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford University Press.

Forero, R., Nahidi, S., De Costa, J., Mohsin, M., Fitzgerald, G., Gibson, N., McCarthy, S., & Aboagye Sarfo, P. (2018). Application of Four-Dimension Criteria to Assess the Rigour of Qualitative Research in Emergency Medicine. *BMC Health Services Research*, *18*(1), 1–11.

Friese, S. (2012). Qualitative Data Analysis with ATLAS.ti. London: SAGEPublication Ltd.

Gabriel, G. M. (2023). A History of Management of the Intangible Cultural Heritage Resources within the Sukuma: A Case of Magu District from 1860s to 2020s. *International Journal of Research and Innovation in Social Science*, *7*(11), 828-854

Gwet, K. L. (2012). *Handbook of Inter-rater Reliability: The Definitive Guide to Measuring the Extent of Agreement among Multiple Raters MD*. Advanced Analytics Press.

Gregory, A. (2024). A Historical Reflection in Sukuma Land, Tanzania. *East African Journal of Education and Social Sciences Studies*, 5(4), 397–405.

Gregory, A., Luvumwa, P., Msuya, V., & Abel, M. (2024). African Indigenous Knowledge Systems in the Contemporary Era: A Historical Reflection in Sukuma Land, Tanzania. *East African Journal of Education and Social Sciences*, *5*(4), 94-102.

Jackson, H. (2014). *Matumizi ya Lugha ya Kisukuma katika Kiswahili cha Mazungumzo* (Doctoral Dissertation, University of Dar es Salaam).

Khamis, A. A na wenzake. (2008). *Utamaduni wa Mzanzibar*. BAKIZA.

Masanja, T. (2016). The Edifying Role of Wasukuma Mythical Narratives and the African Concepts of Idealism and Realism. Master's Thesis, University of Dar es Salaam.

Matteru, M. D. (1983). "Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili, katika Fasihi": *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili.* TUKI. UK 26-37.

Mbarouk, M. J. (2015). *Athari za Sayansi na Teknolojia katika Hadithi za Watoto: Mifano ya Ngano kutoka Wilaya ya Micheweni Pemba* (Doctoral Dissertation, Chuo Kikuu cha Dodoma).

Mbunda, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Educational Publishers Ltd.

Mlacha, S. A. K. (1995). Fasihi simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba, katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. TUKI. Uk. 16-26.

Mnenuka, A. (2020). Mizimu katika Ngano za Kiafrika: Uchambuzi wa Ngano Teule. *Mulika Journal*, 39, 1-19.

Mulokozi, M. M. (2006). "Fasihi ya Kiswahili na Utandawazi" katika S. Sewangi na J. Madumulla (Wah.) Makala ya Kongamano la Kimataifa la Jubilei ya TUKI– 2005: Kuadhimisha Miaka 75 ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1930 – 2005). Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Musembi, N. N., & Mahero, T. (2022). Nafasi ya Fasihi Simulizi katika karne ya 21: Tathmini ya Nyimbo za Jando za jamii ya Wakamba. *Mulika Journal*, *41*(1), 65-78.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Oyoyo, J. O. (2013). *Uhakiki wa Fani katika Ngano Tano za Kiswahili*. University of Nairobi.

Paschal, M. A. H. O. N. A. (2016). *Oral Literature and Preservation of Cultural Heritage of the Sukuma Tribe in Mwanza: A Case Study, Nyamagana District*.

Raphael, S. M. (2015). *Fani ya Methali za Kisukuma katika Uadilishaji wa Watoto na Vijana* (Master's Thesis, University of Dodoma (Tanzania)).

Saanane, C. B., & Faru, S. (2017). From Grinding Hollows to Information Communication Technology through Media in Selecting Prospective Fiancées: Evidence from Wasukuma Socio-Cultural Practices in Tanzania. *International Journal of Geosciences*, 8(8), 1054–1064.

Sengo, T. S. Y. M. (1987). *Fasihi Simulizi*, *Sekondari na Vyuo*. Nyanza Publications Agency.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam University Press.

Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Serengeti Book Shop.

Simiyu, F. W. (2019). Utata katika Uainishaji wa Fasihi Simulizi: Hali ya Sasa na Mustakabali Wake. *Mwanga wa Lugha*, *3* (Toleo Maalum), 223-238.

Songoyi, E. M. (1997). OLT 103 1: Oral Literature 1. Open University of Tanzania.

Taherdoost, H. (2018). Sampling Methods in Research Methodology: How to Choose a Sampling Technique for Research. *SSRN Electronic Journal*, *5*(2), 18–27.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. Focus Publications Ltd.

Wanjala, F. S. (2015). *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa* (Doctoral Dissertation, Kenyatta University).

Yamane, T. (1967). *Statistics: An Introductory Analysis*. 2nd ed. Harper & Row.